

**Jamhuri Ya Muungano Wa Tanzania
Ofisi ya Waziri Mkuu
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.**

HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI



**MPANGO MKAKATI WA MIAKA MITANO WA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI
2010/11 – 2014/15**

YALIYOMO

	Yaliyomo	i
0.0	Muhtasari	iv
0.1	Utangulizi	iv
0.2	Tamko Kuhusu Mwelekeo, Maoteo, Mada, Majukumu ya Halmashauri	iv
0.2.1	Tamko Kuhusu Mwelekeo.....	iv
0.2.2	Tamko Kuhusu Maoteo.....	iv
0.2.3	Mada	iv
0.2.4	Muhtasari wa malengo Mkakati kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.....	iv

SURA YA KWANZA

1.0	Utangulizi	2
1.1	Dibaji	2
1.2	Programu ya Maboresho ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	2
1.3	Mchakato wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.....	3
1.4	Maandalizi ya Mpango Mkakati.....	3
1.5	Mtiririko wa Mada Zinazohusiana na Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.....	3

SURA YA PILI.

2.0	Tamko Kuhusu Mwelekeo, Maoteo, Mada, Majukumu ya Halmashauri	4
2.1	Tamko Kuhusu Mwelekeo.....	4
2.2	Tamko Kuhusu Maoteo.....	4
2.3	Mada.....	4
2.4	Majukumu ya Halmashauri.....	4
2.5	Majukumu kwa Sekta.....	5
2.5.1	Kilimo na Mifugo.....	5
2.5.2	Maliasili.....	5
2.5.3	Ushirika	5
2.5.4	Afya.	6
2.5.5	Maendeleo ya Jamii.....	6
2.5.6	Ustawi wa Jamii.....	6
2.5.7	Elimu Sekondari.....	6
2.5.8	Elimu Praimari.....	7
2.5.9	Maji.....	7
2.5.10	Ardhi.....	7
2.5.11	Ujenzi.....	8
2.5.12	Viwanda na Biashara.....	8
2.5.13	Mipango.....	8
2.5.14	Utawala.....	8
2.5.15	Fedha.....	8

SURA YA TATU		
3.0	Uchambuzi wa Mazingira ya Ndani na Nje.....	9
	• Uchambuzi wa Mazingira ya Nje	
3.1	Utangulizi	9
3.2	Hali ya Mazingira kwa Ujumla na Kikanda	9
3.3	Maendeleo ya Kitaifa.	9
3.4	Mazingira ya Majukumu ya Kila Siku.....	12

SURA NNE.

4.0	Uchambuzi wa mazingira ya Ndani.....	14
4.1	Kanda Kiekolojia.....	14
4.1.1	Sura ya nchi, Udongo, Uoto wa Asili.....	14
4.1.2	Eneo na Matumizi ya Ardhi.....	14
4.1.3	Hali ya Hewa.....	15
4.2	Shughuli za Kiuchumi	15
4.2.1	Madini.....	15
4.2.2	Uvuvi.....	16
4.2.3	Misitu.....	16
4.2.4	Ufugaji Nyuki.....	16
4.2.5	Kilimo.....	16
4.2.6	Mifugo.....	17
4.2.7	Viwanda.....	17
4.3	Manufaa ya Uzalishaji.....	17
4.4	Muundo wa Utawala Halmashauri ya Manyoni.....	17
4.4.1	Muundo wa Kisiasa.....	17
4.4.2	Muundo wa Utawala na Jinsia.....	18
4.5	Matatizo ya Msingi.....	19
4.5.1	Upungufu wa Chakula.....	19
4.5.2	Ukataji miti Holela.....	19
4.5.3	Uharibifu wa Ardhi.....	19
4.5.4	Maradhi Yanayotokana na Maji.....	19
4.5.5	Kipato cha Chini kwa Wakaazi wa Halmashauri.....	19
4.5.6	Miundombinu Hafifu.....	19
4.5.7	Maswala ya Kiutamaduni.....	19
4.5.8	Maswala ya Teknolojia.....	20
4.6	Vyanzo Vikuu vya Mapato vya Halmashauri.....	20

SURA YA TANO

5.0	Fursa na Vikwazo, Viwezeshi, Vikwazo na Maeneo ya Matokeo...	21
5.1	Sekta ya Maji.....	21
5.2	Sekta ya Elimu Secondary.....	22
5.3	Sekta ya Elimu Praimari.....	25
5.4	Sekta ya Afya.	26
5.5	Sekta ya Ujenzi.....	28
5.6	Sekta ya Fedha.....	29
5.7	Sekta ya Utawala.	30
5.8	Sekta ya Biashara na Viwanda.	31
5.9	Sekta ya Mipango.....	32
5.10	Sekta ya Ustawi wa Jamii.....	33

5.11	Sekta ya Kilimo na Mifugo.....	35
5.12	Sekta ya Maliasili.	36
5.13	Sekta ya Ushirika.....	37
5,14	Sekta ya Ardhi.....	37

SURA YA SITA

6.0	MALENGO MKAKATI NA MIKAKATI.....	39
6.1	Sekta ya Kilimo na Mifugo.....	39
6.2	Sekta ya Ushirika.....	39
6.3	Sekta ya Ujenzi.....	41
6.4	Sekta ya Maji.....	42
6.5	Sekta ya Elimu Sekondari.....	44
6.6	Sekta ya Elimu Praimari.....	45
6.7	Sekta ya Maliasili.....	49
6.8	Sekta ya Rasilimali Watu.....	50
6.9	Sekta ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.....	52
6.10	Sekta ya Biashara na Viwanda.....	54
6.11	Sekta ya Mipango.....	56
6.12	Sekta ya Fedha.....	58
6.13	Sekta ya Afya.....	58

SURA YA SABA.

7.0	Mpango na Majukumu ya Utekelezaji na Bajeti.....	61
7.1	Sekta ya Kilimo na Mifugo.....	61
7.2	Sekta ya Ushirika.....	70
7.3	Sekta ya Ujenzi.....	75
7.4	Sekta ya Maji.....	77
7.5	Sekta ya Elimu Sekondari.....	80
7.6	Sekta ya Elimu Praimari.....	82
7.7	Sekta ya Maliasili.....	86
7.8	Sekta ya Rasilimali Watu.....	88
7.9	Sekta ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.....	92
7.10	Sekta ya Biashara na Viwanda.....	97
7.11	Sekta ya Mipango.....	99
7.12	Sekta ya fedha.....	104

SURA YA NANE

8.0	Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini.....	109
8.1	Utangulizi	109
8.2	Utaratibu wa Ufuatiliaji na Tathmini.....	109
8.3	Ufuatiliaji	110
8.4	Tathmini.....	111

0.0 MUHTASARI.

0.1 Utangulizi.

Mpango mkakati wa Miaka mitano wa Halmashauri ya wilaya ya Manyoni unafafanua mwelekeo wa Halmashauri kwa kipindi cha 2010/11-2014/15 kwa kuzingatia mikakati, shughuli na mahitaji ya rasilimali ili kufikia malengo hayo. Maandalizi ya mpango mkakati wa miaka mitano umezingatia utaratibu maalum wa uchambuzi wa hali iliyopo uliotayarishwa kupitia ushirikishwaji wa wadau muhimu wa Halmashauri.

Mwelekeo wa baadae wa halmashauri unafafanuliwa kwa kuzingatia maoteo, shughuli na malengo mkakati, mikakati, shughuli na mahitaji ya rasilimali ili kufikia malengo hayo. Maandalizi ya mpango mkakati wa miaka mitano umezingatia utaratibu maalum wa hali iliyopo na uliotayarishwa kupitia ushirikishwaji wa wadau muhimu wa halmashauri.

0.2 Maoteo, Matamko, Mwelekeo, Mada na Shughuli za Halmashauri

0.2.1 Tamko Kuhusu Mwelekeo wa Halmashauri

Kauli ya mwelekeo wa halmashauri ya Manyoni ni:-

Kuleta maendeleo endelevu kwa kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa kuzingatia na kuwashirikisha wadau wengine wa maendeleo na kuleta uongozi bora katika kuondoa umaskini na njaa iliyokithiri.

0.2.2 Tamko Kuhusu Maoteo ya Halmashauri

Tamko la Maoteo ya Halmashauri ya Manyoni ni:-

Kuwa Halmashauri bora kuliko zote katika ukanda wa kati ambayo inawajali watu wake na kuwahusisha wadau wake na wadau marafilik wa maendeleo katika utoaji wa huduma bora kwa kuzingatia kanuni za kidemokrasia ifikapo 2015.

0.2.3 Mada

Mada ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni inasomeka kama ifuatavyo:-

Halmashauri ni yetu hivyo inatupasa tuwajibike tuwe wawazi, na tutoe huduma zenye ubora wa juu.

0.2.4 MUHTASARI WA MALENGO MKAKATI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI.

- A. Uboreshaji wa huduma na kupunguza maambukizi ya UKIMWI.
- B. Kukamilisha na kudumisha mpango mkakati wa taifa wa kukomesha rushwa.
- C. Kuboresha upatikanaji wa huduma bora za kijamii.
- D. Kuboresha miundombinu ya halmashauri.
- E. Kuwepo kwa utawala na uongozi bora.
- F. Kuwepo kwa uchumi endelevu kwa wakazi wa wilaya ya Manyoni.
- G. Kuboreka kwa huduma za ustawi wa jamii, maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto.
- H. Kuboresha utayari na uthibiti wa dharula na majanga.
- I. Kusimamia rasilimali za kitaifa na mazingira endelevu.

SURA YA KWANZA.

1.0 UTANGULIZI.

1.1 DIBAJI

Mpango mkakati wa Miaka mitano wa Halmashauri ya wilaya ya Manyoni unafafanua mwelekeo wa Halmashauri kwa kipindi cha 2010/11-2014/15 kwa kuzingatia mikakati, shughuli na mahitaji ya rasilimali ili kufikia malengo hayo. Maandalizi ya mpango mkakati wa miaka mitano umezingatia utaratibu maalum wa uchambuzi wa hali iliyopo uliotayarishwa kupitia ushirikishwaji wa wadau muhimu wa Halmashauri.

Mwelekeo wa baadae wa halmashauri unafafanuliwa kwa kuzingatia maoteo, shughuli na malengo mkakati, mikakati, shughuli na mahitaji ya rasilimali ili kufikia malengo hayo. Maandalizi ya mpango mkakati wa miaka mitano umezingatia utaratibu maalum wa hali iliyopo na uliotayarishwa kupitia ushirikishwaji wa wadau muhimu wa halmashauri

1.2 Programu ya maboresho ya halmashauri ya wilaya ya Manyoni

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejizatiti kutoa huduma zenye ubora kwa raia weke, kupita taratibu na mamlaka za serikali za mitaa kulingana na mwelekeo wa serikali wa mwaka 1996 ambao uliandaliwa na inatekeleza ajenda ya maboreha ya serikali za mitaa ambayo mwelekeo wake ni kuimarisha mamlaka za serikali za mitaa ambazo zimechaguliwa kidemokrasia na kutoa huduma kulingana na matakwa husika kulingana na sera ya kitaifa na sheria zilizopo.

- Halmashauri ya wilaya Manyoni ni mionyon i mwa Halmashauri za wilaya 38 zilizopo kwenye awamu ya kwanza ya programme ya maboresho ambayo ilianza mwaka 2002.
- Programu ya maboresho inahusisha hatua 17 kwa mtiririko wa hatua kwa hatua kama ifuatavyo.

Hatua ya kwanza- Uandajaji wa kikosi cha maboresho cha Halmashauri.

Hatua ya Pili- Warsha ya kwanza ya wadau.

Hatua ya Tatu- Ukusanyaji wa Takwimu

Hatua ya Nne- Uchambuzi wa Takwimu.

Hatua ya Tano- Warsha ya Pili ya Wadau

Hatua ya Sita- Utayarishaji wa Mikakati na Vigezo vya Utendaji.

Hatua ya Saba – Uchambuzi wa utekelezaji wa mikakati wa viashiria vy utekelezaji na Malengo.

Hatua ya Nane- Uandishi wa kitabu cha mpango mkakati.

Hatua ya Tisa – Mapitio ya Halmahauri ya wilaya Manyoni

Hatua ya Kumi- Utekelezaji wa malengo yanayoweza kufikiwa kwa haraka/urahisi.

Hatua ya kumi na Moja- Kuchagua muundo wa halmashauri unaokubalika .

Hatua ya kumi na Mbili – Kuandaa mpango wa utekelezaji.

Hatua ya kumi na Tatu- Kuthibitisha/kupitisha mpango wa utekelezaji.

Hatua ya kumi na Nne- Kuandaa utaratibu wa rasilmali wetu.

Hatua ya kumi na Tano- Kuingiza mpango wa utekelezaji katika mpango wa maendeleo wa Mwaka wa bajeti.

Hatua ya kumi na sita (a) - Utekelezaji wa mchakato wa rasilmali watu.

Hatua ya kumi na sita (b) - Utekelezaji wa mikakati wa utoaji wa huduma.

Hatua ya kumi na saba - Kutekeleza Ufuatiliaji.

1.3. HALI YA MCHAKATO WA MABORESHO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI.

Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ni mojawapo kati ya Halmashauri zinaofanya maboresho kwenye hatua ya kwanza ya mchakato wa maboresho.

- Wakati wa kuandaa mpango mkakati huu halmashauri ilikwisha fikia hatua ya tano ambayo ilikuwa ni ya Warsha ya Pili ya Wadau
Moja ya hatua muhimu ya programu ya maboresho ni uboreshaji wa mpango mkakati wa miaka mitano 2010/11- 2014/15 kwa ajili ya halmashauri. Mpango mkakati una malengo ya kujenga uwezo na kutoa mwelekeo wa wilaya kutekeleza malengo kikamilifu na kwa uhakika. Mchakato wa mpango mkakati ambao ulikuwa shirikishi uliwezesha na wataalam kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma.

1.4 Mchakato ulihusisha hatua zifuatazo.

1 Warsha ya utendaji ya siku tatu iliyohusisha wadau wa halmashauri kwa ajili ya mapitio na makubaliano juu ya:-

- Uwezo wa halmashauri mapungufu ya halmashauri fursa na vikwazo/changamkoto.
- Mambo muhimu na maeneo mahsusi.
- Matarajio na makusudio.
- Malengo mkakati na mikakati.

2. Warsha ya upangaji ya siku 8 iliyohusisha wakuu wa idara wa sekta zote na wasaidizi wao ambayo ilifanaya mapitio juu ya.

- Uwezo wa Halmashauri, mapungufu, fursa na changamoto.
- Mambo muhimu na maeneo muhimu ya maboresho.
- Maoteo na mwelekeo.
- Malengo mkakati na mikakati.

3. Uainishaji wa shughuli za Mpango wa kutekeleza.

4. Uandaaji wa bajeti ya utekelezaji.

5. Mfumo wa Ufuatiliaji na upimaji.

6. Mtiririko wa sura za kitabu cha mpango mkakati.

1.5 Mtiririko wa mada za mpango mkakati Umegawanyika katika maeneo makuu nane ambayo ni:-

- Utangulizi ambao uko kwenye sura ya kwanza.
- Sura ya pili inaonyesha matarajio na makusudio na shughuli muhimu za halmashauri kissekta.
- Sura ya tatu inahusu mapitio ya hali halisi ya halmashauri inayozingatia mambo ya mazingira ya ndani na nje.
- Sura ya nne- inaainisha uwezo, mapungufu, fursa na changamoto katika maeneo muhimu ya halmashauri.
- Sura ya Tano-inaonyesha malengo mkakati na mikakati,.
- Sura ya sita- shughuli, bajeti pamoja na mpango wa utekelezaji.
- Sura ya saba- inaonyesha mpango wa uendeshaji shughuli na bajeti.
- Sura na nane- Inaonyesha Ufuatiliaji na Upiomaji

SURA YA PILI.

2.0 MATAMKO YA MAOTEO, MWELEKEO, MADA NA SHUGHULI ZA HALMASHAURI

2.1 Tamko Kuhusu Mwelekeo wa Halmashauri ya Manyoni ni:-

Kuleta maendeleo endelevu kwa kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa kuzingatia na kuwashirikisha wadau wengine wa maendeleo na kuleta uongozi bora katika kuondoa umaskini na njaa iliyokithiri.

2.2 Tamko Kuhusu Maoteo ya Halmashauri ya Manyoni ni:-

Kuwa Halmashauri bora kuliko zote katika ukanda wa kati ambayo inawajali watu wake na kuwahusisha wadau wake na wadau marafilik wa maendeleo katika utoaji wa huduma bora kwa kuzingatia kanuni za kidemokrasia ifikapo 2015.

2.3 Mada

Mada ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni inasomeka kama ifuatavyo:-

Halmashauri ni yetu hivyo inatupasa tuwajibike tuwe wawazi, na tutoe huduma zenye ubora wa hali ya juu.

2.4 Majukumu ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ni:-

- Kuhakikisha utekelezaji wa sheria sera na kanuni.
- Kutoa huduma bora na endelevu kwa mtindo shirikishi na kufuata utawala bora ili kuondoa umaskini.
- Kudumisha na kuboresha amani na utawala bora ndani ya mipaka yake.
- Kuboresha huduma za maendeleo ya jamii na uchumi kwa watu wote ndani ya mipaka ya Halmashauri.
- Ili kuboresha sheria namba 7 ya 1982 kifunga kidogo cha 111 shughuli za msingi ni.
 - (a) Kuainishsa aman, utulivu na utawala bora.
 - (b) Kuainisha na kuendeleza ustawi wa jamii na uchumi wilayani.

Ili kukamilisha majukumu yaliyotajwa hapo juu Halmashauri itatakiwa kufanya yafuatayo:-

- (i) Kugawa mamlaka ya kisiasa, kifedha na kiutawala kwenye ngazi za chini za halmashauri kwa mfano kata, vijiji na vitongoji.
- (ii) Uendelezaji ushirikishwaji wa jamii katika kutoa maamuzi kidemokrasia katika nyanja zote zinazowahusu.
- (iii) Kuiwezesha halmashauri kujitegemea kwa kutafuta vyanzo vyake vya fedha/mapato ambavyo vitawezesha kutoa huduma endelevu na kuwajibika kifedha kwa jamii na watumishi wa serikali.

2.5. MAJUKUMU KISEKTA.

2.5.1 Kilimo na Mifugo.

- Kutoa huduma za ugani katika kilimo na mifugo kwa jamii.
- Kudhibiti magonjwa ya mlipuko kwa mifugo na wadudu waharibifu.
- Kuhakikisha ubora wa mazao ya kilimo na mifugo
- Kuakikisha wa mkakati wa mapinduzi ya jamii (kilimo kwanza) unatekelezwa kikamilifu.
- Kuhusishwa sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali katika utoaji wa huduma za jamii katika kilimo kwanza.
- Kuwaelimisha wakulima na wafugaji juu ya sera, sheria na kanuni.
- Kuinua kiwango cha matumizi ya vitendea kazi vya uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo.
- Kutoa taarifa/habari za uhakika kuhusu matarajio ya hali ya hewa.
- Kutoa huduma ya kitaalam ya umwagiliaji kwa jamii kwa njia shirikishi.

2.5.2 MALI ASILI.

- Kuinua kiwango cha hifadhi ya matumizi endelevu ya mali asili kama vile:-
 - Uwandikishaji wa hifadhi ya Misitu kwa ajili ya Halmashauri, Vijiji vikundi na Watu binafsi.
 - Uanzishwaji wa hifadhi ya misitu kwa ajili ya Halmashauri, vijiji vikundi na watu binafsi.
 - Uanzishwaji wa hifadhi ya nyuki kwa makundi yaliyotajwa hapo juu.
 - Uanzishwaji wa maeneo ya hifadhi ya wanyama pori.
 - Uendelezaji wa ufugaji bora wa nyuki.
 - Uendelezaji wa ufungaji wa samaki.
- Kusimamia utekelezaji wa sera sheria na sheria ndogondogo kisekta.
- Kuboresha kiwango na msingi wa mazao ya mali asili.
- Kulinda hifadhi za wanyama pori.
- Kuanzisha na kuendeleza kumbukumbu za halmashauri za mali asili.

2.5.3 USHIRIKA

- Kuunga mkono juhudi za kuendeleza elimu ya ushirika kwa wanachana viongozi na jamii kwa ujumla.
- Ukaguzi wa vyama vya ushirika katika hatua mbalimbali.
- Uhamasishaji na utekelezaji wa sera ya ushirika ya mwaka 2002 ya sheria na sheria ndogo ndogo za 2003.
- Uanzishaji wa maboresho ya vyama vya ushirika na uhamasishaji kijinsia, uanzishaji na uendelezaji wa vyama vyama vya akibba na mikopo (SACCOS) na vyama vingine kwa ajili ya kusudio la kuondoa umaskini.
- Uanzishaji wa benki za jamii (Vicoba)
- Kuhusisha SACCOS na vyama vingine vya ushirika na mashirika ya kifedha.

2.5.4 AFYA.

- Kupunguza vifo vya mama wa watoto.
- Kuzuia milipuko ya magonjwa ambukizi kama vile malaria, kipindupindu na uti wa mgongo.
- Kupunguza maradhi yatokanayo na UKIMWI na magonjwa ya zinaa.
- Kuhakikisha upatikanaji na usambazaji wa vifaa vya afya na dawa.
- Kutekeleza sera, kanuni na taratibu za tiba.
- Kutoa matibabu kwa wagonjwa wa nje na ndani ya hospitali.
- Kutoa huduma za kinga na kuendeleza mazingira.
- Kuendesha mafunzo ya afya kwa jamii.
- Kuboresha mfuko wa huduma kwa Jamii.
- Kuwezesha ujenzi wa zahanati katika kila Kijiji na vituo vya Afya katika kila kata.
- Kuanzisha vituo vipya vya upimaji UKIMWI kwa hiari.
- Kuboresha elimu ya mpango wa uzazi.
- Kuendesha ukaguzi wa maduka ya madawa.
- Kuendesha ukaguzi wa maeneo ya kuhifadhia vyakula.

2.5.5 MAENDELEO YA JAMII.

- Kuinua uwezo wa shughuli za kijamii kiuchumi na ushirikishwaji katika maendeleo.
- Kuhakikisha matumizi endelevu ya mali asili.
- Kuiwezesha jamii katika kuainisha mahitaji yao.
- Kutekeleza sera na kanuni za mwendeleo ya jamii.
- Kuondoa umaskini kupitia uanzishwaji wa vikundi vya kiuchumi vya wanawake.
- Kuelimisha jamii juu ya matumizi ya teknolojia sahihi; mfano matumizi ya majiko yanyo okoa nishati, uvunaji wa maji ya mvua, matumizi ya matoroli, mizinga ya nyuki ya kisasa na uongezaji wa thamani wa mazao.
- Kuunganisha shughuli za watoto na jinsia kwenye jamii.
- Kuelimisha/kuhamasisha jamii juu ya ujenzi wa nyumba bora.

2.5.6. USTAWI WA JAMII.

- Kutoa ushauri na saha kwa familia.
- Kuhakikisha wasiojiweza wanapatiwa huduma muhimu.
- Kuwasimamia wananchi walio kwenye matazamia warekebishe tabia zao.
- Kusimamia vituo vya malezi vya watoto wadogo, wa mitaanki, wazee na wasiojiweza.

2.5.7. ELIMU.

(A) Sekondari.

- Kuendelea kuondoa ujinga wa kusoma, kuandika na kuhesabu.
- Kuhakikisha wanafunzi wanaofaulu mitihani yao Kidato cha nne na cha sita:

- wanaoandikishwa kwenye Elimu ya juu na ufundi na kuhitimu masomo yao
- Kuhakikisha kuwa Elimu ya watu wazima inatolewa kikamilifu na kuweka mazingira bora ya ufundishaji na utoaji elimu
- Kusimamia na kuthibithi miiko ya walimu na nidhamu kwa wanafunzi.
- Kusimamia na kuweka mazingira bora ya ufundishaji na utoaji Elimu
- Utekelezaji sera ya Taifa ya Elimu, sheria na kanuni.

5.8 ELIMU.

(B)Elimu Ya Msingi.

- Kuondoa ujinga wa kusoma, kuandika na kuhesabu.
- Kuhakikisha wanafunzi wanaofaulu mitihani yao ya darasa la saba:
 - wanaoandikishwa kwenye Elimu ya sekondari na ufundi na kuhitimu masomo yao
 - Kuhakikisha kuwa Elimu ya woru wazima inatolewa kikamilifu na kuweka mazingira bora ya ufundishaji utoaji elimu
 - Kusimamia na kuthibithi miiko ya walimu na nidhamu kwa wanafunzi.
 - Kusimamia na kuweka mazingira bora ya ufundishaji utoaji Elimu
 - Kutekelezaji sera ya Taifa ya Elimu, sheria na kanuni

2.5.9 MAJI.

- Kutoa huduma ya maji safi na salama kwa jamii mjini na vijijini.
- Kufanya utafiti kwa ajili ya upatikanaji wa rasilimali maji, ubora na utoshelezaji wake.
- Kuhakikisha utekelezaji wa sera ya Taifa ya maji, sheria, kanuni na sheria ndogondogo zinafuatwa.
- Kukusanya takwimu za haidrologia na kuziungaminsha .
- Kuhifadhi vyanzo vya rasilimali maji.
- Kupanga na kutekeleeza uvunaji wa rasilimali mali.
- Kuandaa na kutayarisha maandiko ya miradi ya maji.
- Kuanziha tekinologia rahisi na upatikanaji wa pampu za maji za bei rahisi.
- Kuanzisha na kuendesha mafunzo ya tekinologia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Kushirikiana na wadau wengine katika utoaji wa huduma ya maji.

2.5.10 ARDHI.

- Kuondoa /kutayarisha ramani kwa ajili ya upanuzi wa mji wa manyoni na vitongoji vyake.
- Kutayarisha ramani na kuhakikisha zinathibitishwa kisheria.
- Kuhakikisha ujenzi holela unakomeshwa mara moja.
- Kutoa Elimu kwa jamii ili kuelewa sheria ya ardhi na 4 na 5 ya 1999.
- Kuboresha matumizi ya mpango wa Ardhi.
- Kuiwezesha “PLUM” kufanaya utafiti utafiti ili kutoa hati miliki za kimila kwa jamii.

2.5.11 UJENZI.

- Kutayarisha na kutekeleza mipango endelevu ya ujenzi wa barabara bora na ukarabati unaohusisha wadau wote.
- Kutoa ushauri na kusimamia mitambo na magari ya serikali.
- Kutoa ushauri na kusimamia ujenzi wa majengo binafsi na ya serikali katika wilaya.
- Kushauri jinsi ya kuweka umeme katika majengo ya umma.
- Kuhakikisha kwamba sheria, sheria ndogo ndogo na kanuni zinazohusu usalama wa barabara, majengo na mitambo vinafuatwa na kutekelezwa ipasavyo.

2.5.12 VIWANDA NA BIASHARA.

- Kutoa Elimu kwa jamii ya wafanya biashara jinsi ya kuanzisha biashara endelevu na mikakati ya utafiti wa masoko.
- Kuendesha mafunzo ya jinsi ya kusimamia biashara na matumizi ya sera, sheria na sheria ndogondogo.
- Kuhakikisha kila mfanyabiashara analipa kodi na ushuru kulingana na biashara yake.

2.5.13 MIPANGO.

- Kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo na kiuchumi.
- Kupanga, kuratibu na kufuatilia miradi yote katika wilaya.
- Kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali zinazopatikana wilayani.
- Kuunganisha na kuandika taarifa za robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima zinazohusu utekelezaji wa miradi.
- Kusimamia matumizi ya miradi ya maendeleo wilayani.
- Kufanya utafiti wa mafunzo ya kijamii na kiuchumi.
- Kuanzisha benki ya takwimu za wilaya.
- Kufuatilia na kupima miradi yote ya maendeleo ya wilaya.

2.5.14 UTAWALA.

- Kutekeleza sheria za kazi, taratibu, kanuni, nyaraka na maagizo mbalimbali.
- Kuhamasisha na kuratibu mafunzo kwa watumishi wa halmashauri
- Kujaza nafasi zilizo wazi
- Kusimamia wafanyakazi wa halmashauri.
- Kuratibu viwango vya utendaji kazi za watumishi wa halmashauri.
- Kuhifadhi na kurekebisha mfumo wa habari za rasilimali watu.
- Kusimamia utendaji wa masijala ya wazi na ya siri ya halmashauri.

2.5.15 FEDHA.

- Kufanya ufuatiliaji wa makusanyo ya mapato ya halmashauri yatokanayo na vyanzo vyake.
- Kutunga na kusimamia sheria ndogo ndogo za fedha za halmashauri.
- Kutayarisha taarifa za maendeleo za fedha za mwezi, robo mwaka nusu mwaka na mwaka mzima.
- Kuhakikisha kila idara ya halmashauri inatumia mafungu ya fedha kulingana na jinsi ilivyopitishwa kwenye bajeti”

- Kutambua vyanzo vya fedha ili kupanua wigo wa mapato ya halmashauri.

SURA YA TATU.

3.0 UCHAMBUZI WA MAZINGIRA YA NJE NA NDANI YA HALMASHAURI.

3.1 Utangulizi.

Mazingira ya nje ya Halmashauri ya wilaya ya Manyoni yahahusu hali na vipengele vyote vya nje ya halmashauri ambavyo vinaweza kusabaisha maendeleo yake kufanikiwa au kutofanikiwa. Sura hii inapitia mazingira ya nje ili kutambua mambo muhimu yanayohusu uwezo, mapungufu fursa na changamoto za halmashauri. Kwa kuzingatia misingi ya fursa na vikwazo, mambo muhimu ya kimkakati na maeneo muhimu ya utekelezaji ambayo yanatoa mwelekeo wa mpango mkakati yameanzishwa.

3.2 Mazingira ya Jumla na Kikanda.

A. Tekinologia ya habari na Mawasiliano.

- Kuongeza/kupanua majukumu ya tekinologia ya habari na mawasiliano. Fursa zilizoletwa na tekinologia ya habari na mawasiliano, i.e. tovuti, kompyuta, zinahimiza matumizi makubwa ya tekinologia hiyo mpya katika utendaji wa halmashauri. Matumizi ya tekinologia mpya yataunganisha halmahauri na ulimwengu na hivyo kuleta maendeleo kwa haraka. Hivyo miundo muhimu ya hiyo tekinologia mpya niya msingi kuendelezwa na kuboreshwa katika wilaya.

B. Mifumo ya Kimataifa.

- Mifumo ya Biologia anuwai, ukuwaji wa uwajibikaji wa jamii duniani kuhusu maendeleo endelevu yalichochea ukuwaji wa mifumo ya biologia anuai. Ukuwaji huu unawakilisha fursa ya pekee ya maendeleo katika mfumo wa Biologia anuai, na matumizi endelevu ya vipengele vyake na mgawanyo sawa wa faida zinazotokana na matumizi ya rasilimali hai. Tanzania inawajibika katika mfumo wa baologia anuai.
- **Mazingira ya Maendeleo.**
Tanzania ilishiriki katika mkutano wa kimataifa wa mazingira wa maendeleo uliofanyika Riodejeneiro 1992 ambao ulisisitiza umuhimu wa kuunganisha matatizo ya mazingira na maendeleo ya uchumi na walitengeneza Agenda ya 21 ya programu kamili ya hatua ya kutengeneza msingi wa uhusinao mpya wa kilimwengu wa kukomesha na kurejesha hali nzuri iliyosabaisha kuharibika kwa mazingira na kuleta maendeleo endelevu katika nchi zote.

3.3 MAENDELEO KITAIFA.

A. Programu ya Maboresho ya Watumishi wa Umma.

Utumishi wa umma Tanzania upo katika mchakato wa maboresho na mpito katika juhudi za kuungamisha/kujenga utamaduni bora na kuupa ummahuduma zinazolingana na thamani ya fedha. Uutamaduni huu mpya na maboresho unazingatia mambo ya thamani ambayo ni pamoja na ubora, uzalishaji, ubunifu, uaminifu, uwajibikaji, nidhamu na utaalumu. Mtazamomuhimu wa hizi juhudi ni kuongeza uwezo katika usimamizi na uongozi wa shughuli za umma na kutoa mchango mzuri kwa ajili ya kufanikisha malengo ya maendeleo ya Taifa na matarajio ya malengo ya 2025.

B. Matarajio ya Tanzania 2025

Mamlaka ya halmashauri ya wilaya ya Manyoni inahusishwa na malengo ya Tanzania ya muda mrefu na matarajio ya Mwaka 2025 ambayo yanalenga kwenye mambo yafuatayo.

- Huduma zenye ubora wa hali ya juu.
- Amani, uvumilivu na umoja.
- Utawala bora.
- Uwezo
- Ushindani kinchi.

C. MAMBO YANAYOHUSU UCHUMI NA SIASA.

Uchumi wa kitanzania umekadiriwa kuendelea kukua kwa kiwango cha asilimia 5 kama ilivyojulikana miaka ya nyuma. Inakadiriwa kwamba miaka 5 ijayo uchumi wa Taifa utakuwa kwa asilimia 6. Pamoja na matumaini hayo uchangiaji kwa sekta ya umma bado unabaki kuwa mdogo kwa kipindi chote cha mpango wa miaka 5 kutokana na mahitaji mbalimbali ambayo ni pamoja na deni la nje. Mwelekeo huu utasababisha matokeo hasi kwenye uwezo wa halmashauri ya wilaya ya Manyoni katika kukamilisha malengo yake.

D. Mpango wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA)

MKUKUTA ulipangwa ili kutekeleza matarajio ya maendeleo ya Tanzania ya 2025 na unalenga kupunguza umaskini, njaa, maradhi na kuondoa ujinga, uharibifu wa mazingira na tofauti za kijinsia ifikapo 2025. MKUKUTA unachanganua mkakati wa kupunguza umaskini na kuimarisha maendeleo endelevu kwa kufuata/kulingana na maeneo muhimu yafuatayo:-

- (i) Kukuza na kupunguza umaskini wa kipato.
- (ii) Kuboresha hali ya maisha na jamii kwa ujumla.
- (iii) Utawala bora na uwajibikaji.

E. SHERIA HUSIKA.

(a) Sheria ya usimamizi wa mazingira namba 20 ya 2004

Sheria ya usimamizi wa mazingira namba 20 ya 2004 inatoa umuhimu wa mwelekeo juu ya hali halisi ya mazingira kwa sasa na baadae ikiwa ni pamoja na uchafuzi wa maji, hewa, ardhi na utupaji wa taka zenye madhara.

Halmashauri ya wilaya ya manyoni ikiwa ni moja ya wadau muhimu inalazimika kuchangia kuunda na kutekeleza na kusimamia uhifadhi wa mazingira.

(b) Sheria ya hifadhi ya wanyama pori namba 12 ya 1974)

Vipau mbele vya sheria vinazingatia uanzishaji wa maeneo ya hifadhi kuzuia uwindaji haramu, na uporaji wa wanyama. Sheria vile vile inazuia uchomaji na ukataji ovyo wa miti na mapori.

(c) Sheria ya Usambasaji Maji Usafi namba 12 ya 2009)

Sheria hiyo inalenga usimamizi endelevu na inajikita katika utoaji huduma za usambazaji maji usafi na kwa taratibu na kuzingatia sera za kitaifa za mamlaka ya usambazaji maji safi na salama na mashirika binafsi ya usambazaji maji kwa wananchi.

(d) Sheria ya uvuvi ya 2003.

Sheria hii inalenga katika usimamiaji na usisitizaji wa uvuvi kufuatana utamaduni wa aslia ya uvivu na uhifadhi wa samaki pamoja na mazalia zake.

(e) Sheria ya Misitu namba 14 ya 2002

Sheria hii inasisitiza maendeleo na utekelezaji mipango ya usimamizi wa misitu inaoshirikisha jamii ikiwa ni pamoja na uhifadhi wa misitu ya vijiji na jamii pamoja na utoaji wa leseni ya matumizi ya misitu. Kwa nyongeza sheria inahakikisha uhifadhi wa viumbe hai anuai kupitia hifadhiya misitu, vyanzo vya maji hifadhi rutuba na ardhi

(f) Leseni za Biashara ya 25 mwaka 1972

Sheria inarekebisha shughuli za biashara na inakuza uzingatiaji wa sheria za biashara na kanuni zake katika sekta hiyo.

(g) Sheria ya Ardhi namba 4 ya 1999

Sheria inakusudia kuhakikisha kwamba inaboresha huduma za kijamii zilizoko inatambua matumizi na umiliki wa muda mrefu wa ardhi ambayo yamefafanuliwa kwa kuzingatia sheria husika ili kuwezesha mgawanyo sawa na upatikanaji wa ardhi kwa raia wote. Vile vile inakusudia kuhakikisha kwamba ardhi inatumika kiuzalishaji zaidi na kwamba matumizi hayo yenaleta maendeleo endelevu.

SERA KISEKTA.

(a) Sera ya Maji Kitaifa (2002)

Vipaumbe muhimu ni pamoja na:-

- 1 Ukosekanaji w amaji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya mjini na vijijini.
- 2 Uchakavu wa mifumo unaosababisha kuzalishwa maji yasiyo safi na salama kusababisha bei ya maji kuwa juu.
- 3 Ushirikishwaji wajamii katika kamati za maji.
- 4 Uhifadhi wa rasilimali maji
- 5 Lengo ni upatikanaji wa maji safi na salama umbali wa mita 400 ifikapo 2025.

(b) Sera ya Kitaifa ya Nishati (2003)

Sera inasisitiza umuhimu wa kuhakikisha upatikanaji wa Nishaji ya uhakika kwa bei nafuu na ulio sawa kwa wote na endelevu ili kusaidia maendeleo ya Taifa.

(c) Sera ya UKIMWI (November 2001)

Lengo la jumla la sera ya Taifa ya UKIMWI ni kutoa mwelekeo kwa sekta zote na wadau wote kwa utaratibu wa mrejesho wa kitaifa kuhusiano na mlipuko wa ugonjwa wa UKIMWI.

(d) Sera ya Taifa ya Elimu (1995).

Sera ya Elimu ya Taifa ya 1995 ina malengo yafuatayo:-

(i) Shule za msingi.

- Kuongeza uandikishwaji wa wanafunzi katika shule za msingi.
- Upatikanaji sawa wa vifaa vya Elimu kwa shule zote za msingi (nyumba, madarasa, madawati, walimu na vitabu)

(ii) **Shule za sekondari.**

- Kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu mitihani ya darasa la saba katika shule za msingi wanajiunga na sekondari.
- Upatikanaji sawa wa vifaa vya elemu kwa shule zote za sekondari (nyumba, madarasa, maabara, maktaba, walimu, vitabu na madawati)

(e) **Sera ya Kitaifa ya Afya.**

Sera ya kitaifa ya afya ina madhumuni yafuatayo:

- Kupunguza idadi ya vifo vitokanayo na maradhi yanayoweza kuzuilika na kuongeza miaka ya kuishi kwa Watanzania hadi kufikia miaka 70 kutoka miaka 53 ya sasa.
- Kutoa huduma za afya karibu zaidi wa makazi ya watu kwa kwiano wa watu 100.000 kwa kila Hospitali ya wilaya, watu 10,000 kwa kila zahanati.
- Kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma za afya ni sawa kwa watu wote.
- Kutoa elimu ya afya kwa magonjwa yanayoweza kuzuilika kwa kuimarisha huduma za afya ya msingi.

(f) **Sera ya Taifa ya Kilimo na Mifugo.**

Sera ya Taifa ya kilimo na mifugo inalenga kutoa huduma bora kwa taratibu zaidi kwa wananchi kusudi kuongeza mazao ya kilimo na mifugo na kwa kushirikiana na sekta binafsi.

(g) **Sera ya Taifa ya Barabara.**

Sera ya taifa ya barabara inalenga kuweka kipaumbele cha kwanza katika uboreshaji wa miundo mbinu na utoaji wa matengenezo makubwa ya barabara kuu wa mkoa, wilaya na vijiji.

(h) **Sera za Kutaifa za Maliasili na Mazingira.**

Sera za mali asili na mazingira zinasisitiza ushirikishwaji wa watu wote katika kuhifadhi, kukuza na uvunaji endelevu wa mali asili.

(i) **Sera ya Taifa ya Biashara na Viwanda.**

Madhumuni ya sera ya Taifa ya viwanda na biashara ni kuwezesha Watanzania kutumia teknolojia za kisasa kwa kutambua njia inayowezekana kufanya biashara ya ushindani wa biashara za nje kwa ajili ya kufikia lengo la kuondoa umaskini.

(j) **Sera ya Kitaifa ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

Sera ya kitaifa ya maendeleo ya jamii na jinsia na watoto inamini kwamba kila mwananchi anayohaki ya kumiliki mali, kushiriki katika shughuli za kimaendeleo na haki sawa ya kupata huduma za kijamii.

(k) **Sera ya Kitaifa ya Ushirika (2002)**

Sera ya kitaifa ya ushirika inalenga katika kuanzisha, kuimarisha na kuendeleza na kujenga ushirika endelevu ili kutimiza matakwa ya watu ya kijamii na kiuchumi.

3.4 Majukumu ya Kila Siku.

Majukumu (yaani shughuli za halmashauri za kila siku zinazounganisha sekta mbali mbali) ni pamoja na serikali kuu (serikali za mitaa na tawala za mkoa, katibu tawala mkoa RAS), katibu tawala wilaya (DAS) mashirika rafiki na mashirika ya watu binafsi kuwa ndiyo washiriki wakuu.

(a) Msaada wa Serikali.

Serikali kuu imejitoa kusaidia serikali za mitaa ili kukamilisha majukumu yao makuu kupitia misaada mbalimbali ya kifedha na utalam ili kutoa ushauri wa kuratibu utengenezaji wa sera, usimamiaji na tathmini. Vile vile inatoa msaada wa kufanikisha program ya maboresho.

(b) Washiriki Rafiki wa Maendeleo.

Washiriki rafiki wa maendeleo wamefanikisha majukumu muhimu katika maeneo mbali mbali ya halmashauri. Mashirika hayo ni pamoja na shirika la:

(i) AMREF.

Ni shirika linalojihusisha na utoaji misaada kifedha kwa ajili ya shughuli za upimaji, na ushauri nasaha wa virusi vya ukimwi (VVU) kupitia program ya Angaza.

(ii) UNDP

Shirika linalotoa misaada ya fedha kwenye vitengo vidogo vidogo na kutoa elimu ya kujenga uwezo.

(iii) UNICEF.

Inatoa misaada ya kifedha kwa ajili ya kufanikisha chanjo mbalimbali kwa watoto wenye amri wa kwenda shule (CSPD)

(IV) MIBOS (NGO)

Shirika hili linahamisisha na kufanya kazi na jamii za halmashauri ili kupiga vitaumaskini.

(v) TADERO (NGO)

Shirika linatoa huduma za kuwahamashisha jamii kujua madhara ya ulevi wa kupindukia.

(vi) BENKI YA DUNIA.

Msaada wa kifedha katika huduma za utoaji maji safi na salama

SURA YA NNE.

4.0 UCHAMBUZI WA MAZINGIRA YA NDANI.

4.1 KANDA YA KILIMO KIEKOLOJIA.

4.1.1 Sura ya Nchi, Udongo na Uoto wa Asili.

Eneo la kaskazini magharibi la wilaya ambalo linajumuisha kutokea Itigi na Mgandu ni mbuga ambayo imegawanyika katika chemchemi za muda zenye kiasi kidogo cha maji. Udongo wenye rutuba unapatikana kwenye miinuko ambayo ina udongo mweusi wa ufinyanzi unaopatikana katika mabonde yake. Uoto wa asili ni mchanganyilo wa vichaka na mbuga za nyasi.

Eneo linalojumuisha kata za Rungwa, Mgandu kusini na eneo kubwa la kata ya Nkonko nila mwinuko pamoja na mabonde yenye vijito vya maji vinavyotiririka kuelekea mashariki na kuingia kwenye eneo chepechepe la wilaya ya Bahi. Mchanganyiko wa aina mbalimbali za udongo unapatikana kwenye maeneo ya miinuko na mabonde ya sehemu hiyo, uoto wa asili niwa aina ya miti ya miyombo.

Maeneo ya kaskazini mashariki ambayo yanajumuisha karibu kata nzima ya Kintinku kata za Sanza, Sasajila, Majili na maeneo kadhaa ya kata za Manyoni na Makulu ni sehemu ya mbuga zenye mabonde yenye maji yanayotiririka kuelekea maeneo ya wilaya ya Bahi.

Aina ya udongo wenye rutuba wenye rangi kahawiya unaopatika kwenye maeneo ya mwinuko, unabadilika na kuwa wa mvinyanzi (rangi nyeusi) kuelekea sehemu zenye majimaji za wilaya ya Bahi.

Uoto wa asili katika eneo hili unamchanganyiko wa vichaka na mbuga za nyasi pamoja na uoto wa asili wa mimea inayopatikana kwenye mbuga za maji maji.

Eneo la kuzunguka kata za Iseke, Heka, Azimio Chikola na eneo dogo la Nkonko nila mbuga, miinuko na mabonde ambayo yanatiririsha maji yake kusini kuelekea mto wa Ruaha. Udongo wa kahawia unapatikana kwenye maeneo ya miinuko na ule wa Rangi ya mfinyanzi mweusi unapatika katika maeneo ya mabonde ya uoto wa asili na mchanganyiko wa vichaka na mbuga za nyasi.

Eneo ambalo linajumuisha kata za Manyoni, Sanjaranda, Makulu, Ipande, Idoyandole, Aghondi na Makanda ni ya mbuga na udongo wa kichanga wenye rangi ya kahawia katika maeneo ya mwinuko isipokuwa kwenye maeneo machache ambayo yana udongo wa mfinyanzi mweusi. Uoto wa asili niwavichaka vya pekee ambavyo vinajulikana misitu midogo midogo ya Itigi.

Wilaya ya Manyoni ina kanda kuu tatu za kilimo ambazo ni Bonde la Ufa, Mbuga za Miyombo na Sehemu za Miinuko Midogo Midogo.

4.1.2 Matumizi ya Ardhi.

Wilaya ya Manyoni ina eneo la kilomita za mraba zipatazo 28,680 ambazo zinazokadiriwa kuwa ni asilimia 58 ya eneo lote la mkoa wa Singida.

Jedwali na 4.1 linaonyesha hali ya matumizi ya Ardhi.
 Jedwali no 4.1: Matumizi ya Ardhi katika Wilaya ya Manyoni.

Matumizi	Eneo (ha)	Asilimia
Hifadhi ya wanyama pori	1,574,100	55.0
Misitu	858,600	30.0
Kilimo	88,830	3.1
Mifugo	335,470	11.7
Maji	5,000	0.2
Jumla	2,862,000	100

4.1.3 Hali ya Hewa.

(a) Mvua.

Wilaya ya Manyoni ina msimu mmoja tu wa mvua ambao hunyesha kwa kipindi cha miezi 6 kuanzia mwezi Novemba hadi Aprili. Wastani wa juu wa mvua ambao unapatikana katika wilaya ya Manyoni ni Mililita 624 na kuongezeka au kupungua kwa mililita 179. Kwa wastani Mvua hunyesha kwa muda wa siku 49 kwa mwaka na kupungua au kuongezeka kwa siku 15 kwa mwaka. Kwa ujumla upatikanaji wa mvua katika wilaya hii ni mdogo na usiotegemewa.

(b) Kiwango cha Joto.

Kiwango cha wastani cha joto cha kila siku kwa Mwaka ni nyuzi joto 22.0 kiwango cha wastani cha juu na cha chini chakila siku kwa mwezi ninyuzi joto 24.14 (Novemba) na 19.3 (Julai)

(c) Kiwango cha Baridi.

Kiwango cha wastani cha Baridi cha kila siku kwa Mwaka ni asilimia 80.6. Kiwango cha wastani cha juu na cha chini cha baridi kwa mwezi ni nyuzi joto 86 (Februari) na nyuzi joto 73.4 (mwezi Julai)

(d) Myeyuko

Wastani wa juu na wa chini wa myeyuko kwa mwezi ni mm 6.6 kwa siku (Novemba) na 5.2 mm kwa siku (Januari)

(e) Msimu wa Kiangazi.

Wilaya ya Manyoni ina msimu mmoja mrefu wa kiangazi ambao unanza mwezi Mei kila mwaka na kukoma mwezi Oktoba.

(f) Kasi ya Upepo.

Kumbukumbu kuhusu kasi ya upepo inaonyesha kwamba wastani wa kasi ya upepo wa kila siku kwa mwaka ni kilomita 3600 kwa saa. Wakati wa msimu wa upepo (Agosti mpaka Disemba). Kasi ya upepo kuvuma zaidi ya kiwango kilichotajwa.

4.2 Shughuli za Kiuchumi.

4.2.1 Madini.

Aina mbalimbali za madini hupatika katika wilaya ya Manyoni. Madini hayo ni pamoja na gipsam, dhahabu na chumvi. Shughuli hizi za uchimbaji ni pamoja na upatikanaji wa vitu vya ujenzi kama vile mawe, kokoto, mchanga na vitu vingine. Wachimbaji wadogowadogo hufanya shughuli hizi kwa kutumia nyenzo za mikono.

4.2.2 Uvuvi.

Shughuli za uvuvi hufanyika katika maeneo ya Bwawa la Chibumangwa na maeneo yenye majimaji nyakati za msimu wa mvua. Uvuvi hufanyika na wavuvi wadogo wadogo kwa ajili ya kitoweo. Llakini misimu yenye mvua nzuri wauzaji wa samaki huuza samaki kwenye masoko ya nje ya wilaya.

4.2.3 Misitu.

Shughuli za uzalishaji wa mazao ya mbao husaidia baadhi ya wakazi katika wilaya katika kuendesha maisha yao. Kwa mfano 2002 jumla ya mita za ujazo 203 za mbao zenye thamani ya T sh 7,100,00/= zilizalishwa.

4.2.4 Ufugaji Nyuki.

Shughuli za ufugaji nyuki zinafanywa kwa malengo ya kuzalisha asali na nta; kwa mfano 2002 jumla ya kg 75,000 za asali zenye thamani ya Tsh 37,500 zilizalishwa.

4.2.5 Shughuli za Kilimo

Shughuli za kilimo hufanywa katika kata zote 21 za halmashauri. Shughuli za kilimo huzalisha mazao ya chakula na biashara kama mtama, uwele, mpunga na maharage. Mazao makuu ya biashara ni tumbaku, uwele, alizeti na karanga.

Jedwali na 4.2 linaonyesha msimu wa uzalishaji wa chakula msimu 2001/ 2002

AINA YA ZAO	UZALISHAJI					
	2000/01			2001/02		
A.Mazao ya Chakula	Eneo (ht)	Mt	Thamani (000 Tsh)	Eneo (ht)	Mt	Thamani (000Tsh)
Mtama	17,189	10,313	680,658	44,717	20,687	1,939,406
Uwele	884	884	58,933	1075	1,365	95,550
Mahindi	26,040	31,248	3,906,000	25624	44,717	409,712
Mpunga	480	864	388,800	1413	3,676	1,102,800
Maharage	5,374	4,299	1,504,650	4,057	4,060	1,218,000
Ndizi	2853	20,588	3,088,200	3,276	17,890	1,789,000
Jumla	52,820	64,196	9,627,241	80,162	92,395	6,554,468
B. Mazao ya Biashara						
Tumbaku	846	508	264,160	847	685	479,500
Ufuta	2,963	2,222	1,388,750	3,336	3,181	1,431,450
Alizeti	243	80	8,000	485	436	31,392
Karanga	7,363	4,417	2,808,500	7,526	6,103	3,661,800
Dengu	1,085	1,085	488,025	1,142	1,142	513,900
Jumla	12,500	8,312	4,957,615	13,336	11,547	6,118,042

Chanzo: Idara ya Kilimo na Mifugo, Wilaya Manyoni

4.2.6 Mifugo

Uzalishaji wa mifugo kama vile g'ombe, mbuzi, kondoo na kuku umeongeshwa katika jedwali 4.3. Vielelezo vinaonyesha kwamba uzalishaji wa ng'ombe na kuku unachangia asilimia kuwa kwenye kipato cha wafugaji.

Jedwali 4.3: Uzalishaji wa Mifugo 2002

Aina ya Mifugo	Aina ya zao	Kiasi	Thamani
Ng'ombe	Nyama(kilo)	232,250	232,250,000
	Maziwa (lita)	11,997,666	179,964,900
	Ngozi (idadi)	929	2,322,500
	Jibini (kilo)	96,160	184,320,000
Mbuzi/kondoo	Nyama (kilo)	10,380	15,570,000
	Ngozi (idadi)	692	173,000
Kuku	Mayai (idadi)	1,868,340	130,783,800
	Nyama (Kilo)	648,000	1,296,000,000
Bata	Mayai (idadi)	78624	762,400
	Nyama (kilo)	360	720,000

Chanzo: Idara ya Kilimo na Mifugo, Wilaya Manyoni

4.2.7 Viwanda.

Shughuli za viwanda ambazo zinachukua nafasi ya viwanda vidogo vidogo ambavyo vimejumuishwa viwanda 9 vya kutengeneza mafuta na kiwanda kimoja na kutengeneza chaki. Uatikanaji wa takwimu kuhusu uzalishaji kuhusiana na sekta hii alikuwa mgumu sana kutokana na utunzaji duni wa kumbukumbu katika halmashauri ya wilaya.

4.3 Matokeo ya Uzalishaji.

Kiasi cha uzalishaji kilichotajwa hapo juu kina mchango mkubwa katika upatikanaji wa kazi na mapato katika wilaya. Wastani wa kipato cha kila mkazi wa wilaya ya manyoni kinakadiriwa dola za kimarekani 170 kwa mwaka kutokana na hali hii inaonekana kwamba watu wengi katika wilaya hii wanaishi katika umaskini na watapata maendeleo wanapoweza tu kuvuka mstari wa kimataifa wa kiwango cha umaskini wa dola za kimarekani 750 kwa mwaka.

4.4 Mfumo wa Utawala wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni

4.4.1 Muundo wa Kisiasa.

Wilaya imegawanyika katika Tarafa 5 kata 21 vijiji 75 na vitongoji 314. Kuna majimbo 2 ya uchaguzi ambayo ni Manyoni Mashariki na Magharibi. Kuwa vyama vya siasa 7 ambavyo ni CCM, Chadema, CUF, UPDP, NCCR Mageuzi, UDP na TLP. wa kidemokrasia. Kuna madiwani 21 (kwa kila kata) ambao huchaguliwa kidemokrasis pia kuna madiwani wa vitu maalum 7 ambao ni wanawake.

Kuna wenyeviti 75 wa vijiji ambao wote ni wanaume. Kuna wenyeviti 314 wa vitongoji ambao asilimia (93) ni wanaume na 21 ni wanawake (ambao ni 7%). Wawakilishi wote wanatoka chama cha mapinduzi (CCM)

Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya ya manyoni ni kiongozi wa halmashauri na mwenyekiti wa madiwani wote. Mkurugenzi mtendaji wa wilaya ndiye mtendaji mkuu na katibu wa baraza la madiwani. Baraza la madiwani ndiyo lenye uamuzi/mamlaka ya mwisho kama ilivyoonyesha katika sheria namba 7 ya serikali za mitaa ya 1982. Kuna familia mbalimbali ambazao zipo chini ya halmashauri kama vile halmashauri ya maendeleo ya kata ambayo huongozwa na mwenyekiti wa kuchaguliwa wa madiwani wa kata husika. Katibu mtendaji wa kata ndiye mtendaji mkuu na ni katibu wa kamati ya maendeleo ya kata husika.

Wajumbe wa kamati ya maendeleo ya kata ni wenyekiti wa vijiji waliochaguliwa katika kata zinazohusika. Wataalam wa ugani katika kata zote ni wajembe wa kukaribishwa. Na katika ngaza ya kiji ambayo inaongozwa na mwenyekiti wa kuchaguliwa wa kijiji na katibu wa kijiji ni katibu wa Baraza la kijiji.

Serikali ya kila kijiji ina wajumbe 25 wa kuchaguliwa kutoka kwenye kijiji husika na wataalam wa ugani wanaofanya kazi katika vijiji hivyo ni wajumbe kutokana na nafasi zao.

4.4.2 Muundo wa Utawala na Jinsia.

Katika utawala wa halmashauri mkurugezi mtendaji wa wilaya huteuliwa na waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa na ndiye mtendaji mkuu wa halmashauri. Wakuu wa idara 14 na wakuu wa vitengo 28 (jedwali 4.4) humsaidia mkurugenzi mtendaji wa wilaya. Halmashauri ina jumla ya waajiriwa 1260 ambao kati yao 783 (62%) ni wanaume 477 (38) ni wanawake.

Jedwali no 4.4: waajiriwa kwa sekta na jinsia.

SEKTA	WAAJIRIWA			Jinsia Ya Wakuu Wa Idara.	
	ME	KE	Jumla	Me	Ke
Utawala	72	38	110	V	-
Mipango	4	-	4	V	-
Fedha	13	5	18	-	-
Elimu	416	219	680	V	V
Maji	25	10	35	V	-
Afya	88	184	272	V	-
Kilimo/mifugo	45	3	48	V	-
Ushirika	3	1	4	V	-
Biashara	2	-	2	V	-
Ardhi	4	-	12	V	-
Maendeleo ya jamii	7	5	2	-	V
Utamaduni vijana na michezo	2	-	49	V	-
Ujenzi	42	7	20	V	-
Maliasili	15	5	1,260	V	-
Jumla	783	477		12	2

Chanzo: Idara ya Utumishi, Wilaya Manyoni

Halmashauri inaendesha kazi zake kupitia kamati 4 za kudumu ambazo ni kamati za fedha mipango na utawala, afya, Elimu, na maji. Ujenzi maliasili na mazingira na UKIMWI zinawakilishwa.

4.5 Matatizo Makubwa.

Matatizo makubwa ya maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ni kama yafuatavyo.

4.5.1 Upungufu wa Chakula.

Uzalishaji mdogo wa sekta ya kilimo ambao unasababishwa na ukame ambao matokeo yake ni upungufu wa mazao ya chakula kama vile mahindi ambayo ni chakula kikuu kwa wakazi wengi wa wilaya ya Manyoni.

4.5.2 Ukataji Holela wa Misit.

Kuna kiwango kikubwa cha uharibifu wa misitu unaosababishwa na kilimo cha kuhamahama, uchomaji holela wa misitu, ukaushaji wa Tumbaku na matumizi ya nishati ya kuni na mkaa kama vyanzo pekee vya matumizi ya nishati kwa matumizi ya nyumba

4.5.3 Uharibifu wa Ardhi.

Kuna njia nyingi ambazo zinasababisha uharibifu wa ardhi kutokana na kilimo kisicho kuwa cha kitaalam, udhibiti hafifu wa maji ya mvua na idadi kubwa ya mifugo kwenye maeneo madogo.

4.5.4 Magonjwa Yatokanayo na Maji.

Uhaba wa maji safi na salama unawalazimisha baadhi ya watu kutumia maji yasiyosalama ambayo huwasababishia kuenea kwa maradhi yatokanayo na maji yasiyo salama.

4.5.5 Kipato Kidogo cha Wakazi wa Halmashauri.

Shughuli kuu ya wakazi wengi ni kilimo lakini kutokana na mavuno haba au ya mazao ya chakula au ya biashara kipato cha watu wengi huwa ni cha chini. Hali hii inaathiri shughuli za maendeleo ambazo hutegemea zaidi michango ya fedha kutoka kwa wakazi wake.

4.5.6 Miundo Mbinu Hafifu.

Mtandao wa barabara katika wilaya hii haujaendelezwa vizuri. Hakuna mifereji, Barabara wilaya ambazo ni za moram ni km 416 za udongo ni km 569.3. Aina ya barabara ambazo zipo ndani ya wilaya ni barabara kuu km 360, barabara za wilaya km 164 na barabara za vijiji km.491.3. Jumla ya urefu wa barabara zote wilayani km 985.3. Kati ya hizo barabara za wilaya na barabara za vijiji ambazo ni 20% tu hupitika majira yote ya mwaka na barabara zinazobaki ambazo ni asilimia 80 ambazo niza vijiji hazipitiki kabisa wakati wa majira ya mvua hali inayosababisha matatizo makubwa ya usafiri watu wa mizigo.

4.5.7. Shughuli za Utamaduni.

Ujenzi wa mazizi ya ng'ombe karibu/pamoja na makazi ya watu na uhaba wa maji husababisha kuenea kwa ugonjwa wa mtoto wa jicho.

Katika halmashauri ya Manyon. kuna wananchi ambao bado wanashikilia mila porofu za ukeketaji wa wanawake.

4.5.8 Shughuli za Teknolojia.

Kuendeleo kutumia jembe la mkono katika shughuli za kilimo pamoja na utumiaji wa Mbegu zisizokuwa na ubora na mbolea za viwandani vimesabisha kuwepo kwa mavuno hafifu katika wilaya.

4.6 Vyanzo Vikuu vya Mapato ya halmashauri.

Vyanzo vikuu vya mapato ya halmashauri ni pamoja na (ingawaje siyo vyote) kodi ya maendeleo, kodi ya mifugo, kodi ya mazao, ushuru wa masoko, ushuru wa minada pamoja na ushuru mwengine unaojumuhisha leseni za biashara, ushuru wa vilevi ada ya uwindaji wa ada nyingine ambazo zinahusisha zaidi mali na vifaa vya halmashauri.

SURA YA TANO

5.0 FURSA NA VIKWAZO, VIWEZESHI NA MAENEO YA MATOKEO

5.1 SEKTA YA MAJI.

UWEZO	MAPUNGUFU	FURSA	CHANGAMOTO.
Uwepo wa sera za maji na usafi sheria, taratibu na sheria ndogondogo.	Upunguzi wa wafanyakazi.	Uwepo wa seri za maji, usafi, sheria, taratibu na sheria ndogondogo.	Ukame
Uwepo wa maeneo ya vyanzo vya maji.	Ustadi zisizokidhi mahitaji ya kiufundi.	Upatikanaji mkubwa wa rasilmali maji chini ya ardhi.	Uporaji katika miradi ya maji.
Uwepo wa vyazo maji vilivyoendelezwa.	Kukosekana kwa wataalamu katika ngazi ya kata na kijiji.	Uwepo wa sera ya uendelezaji rasilmali maji ya 2006/2025	Ujinga wa jamii husika.
Uwepo wa vyanzo za kufanyia kazi	Utegemezi wa wafadhili.	Uwepo wa wadau	Gharama kubwa za uwekezaji.
	Upungufu wa mafungu ya fedha.	Uwepo wa maji kama bidhaa ya jamii.	Sera za kisekta zisizochangamana.
		Sura ya nchi inayoweza uvunaji wa maji mvua kutoka, kwenye mapaa ya nyumba	Hali mbaya ya kiuchumi ya jamii.
		Upatikanaji wa teknolojia mbadala.	
		Upatikanaji wa nguvu kazi kutoka kwa jamii.	
		Upatikanaji wa chemchem za maji.	

Vikwazo	Viwezeshi
<ul style="list-style-type: none"> • Ukame • Elimu ndogo kwa watumiaji wa maji • Utaalam na vifaa visivyo kidhi haja. • Ukosenaji wa wataalam kwenye ngazi ya vijiji. • Utegemezi mkubwa kutoka kwa wafadhili. 	<ul style="list-style-type: none"> • Hazina ya maji ya mvua. • Wafanyakazi wenye utalaam. • Watumishi wa ugani kutoka sekta nyingine • Nguvu kazi. • Fedha • Sera, sheria na sheria ndogo ndogo • Teknolojia sahihi, mfano pumpu za mkono na za upepo • Kamati za maji • Misitu

Maeneo Muhimu ya Matokeo.

(a) Hali ya hewa na mazingira.

- Ukame.
- Uvunaji wa maji ya mvua.

